

Haki ya taarifa, uwazi na uwajibikaji kwa raia

SHERIA YA HAKI YA KUPATA
TAARIFA, 2016



Kila mtu ana haki ya kupata taarifa.



ISBN:978-9987-710-88-1



Sheria hiyo inatumika Tanzania Bara pekee.

TAARIFA ZA MAENDELEO YA
UJENZI HUU ZINATOLEWA OFISI
YA AFISA TAWALA WA MKOA



Sheria hii inahusu taarifa zilizohodhiwa na taasisi za serikali ama taasisi zinazopokea fedha kutoka serikalini.



Kwa mujibu wa Sheria
ya Haki ya Kupata
Taarifa 2016, "kila
mtu" maana yake raia
wa Tanzania.



TAARIFA ULIYOOMBIA
HATUTOWEZA KUKUPATIA
KWASABABU ZA KIUSALAMA

JESHINI



IDARA ZA
USALAMA

TAARIFA HIZI NI SIRI
ZINAHUSU ULINZI NA
USALAMA WA NCHI



Sheria hii imempa mamlaka mtoa taarifa kutotoa taarifa
ambazo ataona zina viashiria vya kuhatarisha hali ya
ulinzi na usalama wa nchi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya 2016, taarifa zenye viasharia vya kuhatarisha hali ya ulinzi na usalama wa nchi ni kama zile zinzohusu masuala yafuatayo:

- usalama wa Taifa, ulinzi na uhusiano wa kimataifa;
- usalama wa umma;
- uzuiaji, uchunguzi na uendeshaji wa kesi dhidi ya vitendo vya jinai;
- usiri na mambo mengine halali binafsi;
- Maslahi ya uchumi au biashara aidha ya binafsi au umma;
- usawa wa kuhusu mwenendo wa mahakama;
- Asili;
- ukaguzi na usimamizi wa mamlaka za umma;
- Sera za uchumi, fedha na sera za viwango vya kubadilishia fedha wa nchi;
- usiri wa majadiliano ndani ya mamlaka za umma wakati wa uandaaji wa mambo mbalimbali.



MTOA
TAARIFA

MUOMBADI



Mtunza taarifa atakayetoa taarifa zilizozuiliwa na sheria hii, atafungwa kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano.



(Under regulation 11)

ACCESS TO INFORMATION REQUEST FORM

A: PERSONAL PARTICULARS

1. Surname _____ First _____ and _____ Middle _____ Name(s) _____
2. Gender: Male Female
3. Address: _____
4. Phone _____ contact _____ fax _____ (Home): _____
(Mobile): _____

B: REQUEST OF INFORMATION

1. Name of the information holder
2. Date of filing of a request for information
3. Description of the request information
4. Indicate whether you would like to inspect the information and/ or obtain a copy of the information: (tick (v) where applicable)

(i) I want paper copies of documents
(ii) I want electronic copies of documents
(iii) I want to inspect the documents

Date _____ Signature of Applicant _____

FOR OFFICIAL USE ONLY

Dakar,
21st December, 2017
Affairs

PALAMALLAMBA J. A. M. KABORE,
Minister for Constitutional and Legal

Kila muomba taarifa atajaza fomu maalumu inayopatikana kwenye Kanuni za sheria hii, ikiwa na taarifa sahihi za muomba taarifa ambazo zitasaidia mawasiliano naye.

Kwa mtu mwenye ulemavu au asiyejua kusoma na kuandika atawasilisha maombi yake kwa mdomo na mtoa taarifa kuyanakili maelezo yake kwenye fomu maalumu.



NITEGEMEE LINI
MAJIBU YA MAOMBI
YANGU?



MTOA TAARIFA



NITAKUPATIA KWA
MAANDISHI NA NDANI
YA SIKU THELATHINI
KAMA TAARIFA ZIPO
AU HAZIPO



KATIKA MAOMBI YAKO AMBATANISHA
BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA
OFISI YA SERIKALI YA MTAAL WAKO NA
KITAMBULISHO CHA TAIFA.

HAPO PIA HULAZIMIKI
KUTOA TAARIFA ZAKO
BINAFSI ZAIDI YA ZILE
ZA MAWASILIANO



TANI 300 ZA MAHINDI
MCHAFUKOGE ZAHARIBIKA



Mwomba taarifa hatakiwi kupotosha
taarifa alizopewa, ikitokea amepotosha...



... atafungwa kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano.



Mwomba taarifa anaweza kukata rufaa kwa mkuu wa taasisi aliyoomba taarifa hiyo na endapo ombi lake litakataliwa au kaombwa malipo ambayo haoni msingi wake, anaruhusiwa kukata rufaa.





GHARAMA ZA KUDURUFU
NI SH 30,000

Katika mazingira ambayo mwumba taarifa kaombwa malipo ambayo haoni msingi wake, ama hakujibowi taarifa alizoomba, ama kutojibowi ombi lake katika muda uliopangwa kisheria, ana haki ya kukata rufaa

ENDAPO HUJARIDHIKA NA
MAJIBU YA MKUU WA TAASISI HIYO,
UNAWEZA KUKATA RUFAA KWA
WAZIRI





SHERIA YA HAKI YA KUPATA TAARIFA

Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016 (Access to Information Act, 2016) ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 7 Septemba, 2016. Kutungwa kwa sheria hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha haki ya kupata taarifa, kupanua wigo wa taarifa ambayo raia wa Tanzania wanaweza kuipata ili kukuza uwazi na uwajibikaji wa wenyre taarifa pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kutokana umuhimu wa sheria hii, MCT iliona ni vyema kutafuta namna rahisi ya kuifanya sheria hii ieletekele kwa raia ili waweze kuitumia katika kudai haki yao ya kupata taarifa.

MCT iliamua kuchapisha kijitabu hiki baada ya utafiti uliofanywa mwaka 2018 ambao ulionyesha kuwa kuna baadhi ya watoa taarifa ambao ama hawaifahamu sheria hii ama hawaitekelezi kwa makusudi kwa kufahamu kwamba raia wengi hawafahamu uwepo wa sheria hii na pia haki yao ya kupata taarifa.

Kijitabu hiki kimetengenezwa kwa kutumia ya vibonzo ili kutoa tafsiri rahisi isiyo rasmi ya maudhui yaliyopo kwenye Sheria hiyo, ili kumfanya mwananchi aelewe haki zake, taratibu na wajibu wake kama raia wa Tanzania, katika kutafuta taarifa mbali mbali.

Mbali na upungufu uliopo katika sheria hii, tunaipongeza Serikali kwa kuonyesha nia njema katika kuhakikisha kila mwananchi anapata taarifa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na sheria hii.

Kijitabu hiki kinawalenga wananchi wa Tanzania wakiwemo waandishi wa habari.



ISBN:978-9987-710-88-1

Published by Media Council of Tanzania (MCT)
P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2775728/2771947

Mob: +255-784314880
E-mail: media@mct.or.tz
Website: www.mct.or.tz